



Siku moja, mvua
kubwa ilikuwa
imenyesha. Imani
alitazama angani na
kwa mara ya kwanza,
aliona rangi.



Rangi zile zilipendeza sana. Alidhani kuwa mtu fulani alikuwa amefanya kazi kubwa ya kuipaka anga rangi kama vile babake alivyozipaka nyumba.



Alikimbia kumweleza dadake. "Sarah, tazama! Mtu fulani ametupakia anga rangi na kuirembesha."



Lakini Sarah alisema,
“Usiwe mshenzi! Huo
ni upinde. Wewe ni
mdogo nami ni
mkubwa. Ninajua kwa
nini upinde uko
angani. Hebu
nikuonyeshe.”



Alimpeleka Imani
katika bustani ya
wanyama akasema,
"Upinde hautokezei
kwa sababu simba
wananguruma kwa
mara ya kwanza. Wala
hautokezei kwa
sababu tembo
wanazaliwa."



Sarah alimpeleka tena
Imani kwenye bustani
ya maua akasema,
“Upinde hautokezei eti
kwa sababu vipepeo
wameipoteza rangi
yao mawinguni.”



Sarah alimwonyesha
Imani kitabu akasema,
“Vilevile, upinde
hautokezei eti kwa
sababu vifaru
wanakimbia
na kuzitisha rangi.”




“Ninajua kwa nini
pinde hutokezea.
Mama alinieleza, nami
sasa ninakueleza!”
Sarah alimwelekeza
Imani kwenye
uwanja wa michezo.



“Pinde hutokezea angani kwa ajili ya watoto kama mimi na wewe. Siku moja, rangi zilitazama chini kutoka juu na zikafurahia kile zilizoweza kuona.”



"Ziliwaona watoto
wenye rangi ya maji ya
kunde, rangi nyeusi na
rangi iliyo katikati.
Ziliwaza, 'Ni ajabu
ilioje kupendeza kama
watoto hawa
wanavyopendeza.'"



"Rangi hizo ziliuja
pamoja angani
zikajadiliana ambavyo
zingefanya. Ziliamua,
'Tutaweza tu
kupendeza tukiwa
kikundi.'"



“Sasa, huwa
zinaungana pamoja na
kung'ara namna
zinavyoweza. Zina
matumaini ya
kupendeza kama
watoto zinazoona,
watoto kama mimi na
wewe.”